Arusha, Tanzania

Tovuti: www.african-court.org

Simu: +255-272-510-510

AfCHPR
African Court on Human and Peoples' Rights

**MUHTASARI WA HUKUMU**

**AJAYE JOGOO DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**SHAURI NA. 014/2018**

**HUKUMU KUHUSU MAMLAKA NA UKUBALIFU WA SHAURI**

**26 JUNI 2025**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA KUHUSU HAKI ZA BINADAMU NA ZA WATU**

**Arusha, tarehe 26 Juni 2025**: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) leo imetoa Hukumu katika kesi ya Ajaye *Jogoo dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*.

Ajaye Jogoo (Mleta Shauri), raia wa Jamhuri ya Mauritius na Mkurugenzi wa kampuni ya Cimexpan Limited, aliwasilisha Shauri dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Shauri), akidai kufanyika ukiukaji wa haki zake zinazolindwa na Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu (Mkataba). Mleta Shauri alidai kuwa mkataba wake wa makubaliano na Serikali ya Zanzibar kwa ajili ya ujenzi wa "Bustani ya Nyamanzi ya Eneo Huru" ulifutwa kinyume cha sheria, na kusababisha afukuzwe kutoka Tanzania na kukiuka haki zake za kumiliki mali.

Mjibu Shauri hakushiriki katika kesi hiyo, na Mahakama, kwa kutumia Kanuni ya 63 ya Kanuni za Mahakama (Kanuni), ililazimika kuamua endapo inaweza kuendelea kutoa uamuzi wa kesi hiyo moja kwa moja. Kwa kufanya hivyo, Mahakama ilirejelea kwamba Kanuni ya 63 ya Kanuni za Mahakama inaelezea masharti matatu ambayo lazima yatimizwe ili Mahakama itoe uamuzi moja kwa moja: kwanza, upande ulioshindwa kutimiza wajibu wake upewe arifa; pili, hli ya kutotimiza wajibu kwa upande mmoja; na tatu, ama kuwe na ombi kutoka kwa mmoja wa wahusika la kutolewa uamuzi moja

kwa moja, kukiwa hakuna ombi hilo, Mahakama inaweza kutoa uamuzi kwa sababu ya kupata haki.

Kuhusiana na kutoa arifa kwa mhusika aliyeshindwa kutimiza wajibu wake, Mahakama ilibaini kuwa Shauri hili liliwasilishwa ipasavyo kwa Mjibu Shauri mnamo tarehe 30 Julai 2021 na baadaye, mashauri mengine yote yaliyowasilishwa na Mleta Shauri yaliwasilishwa kwa Mjibu Shauri.

Kuhusiana na Mhusika mmoja wapo kushindwa kutimiza wajibu wake, Mahakama ilibaini kuwa Shauri hili liliwasilishwa kwa Mjibu Shauri mnamo tarehe 30 Julai 2021 na Mjibu Shauri alipewa siku 60 za kuwasilisha Majibu yake lakini alishindwa kufanya hivyo ndani ya muda aliopewa. Baadaye Mahakama ilibaini kuwa, Mjibu Shauri alitumiwa mara tatu taarifa za kumkumbusha awasilishe Majibu yake lakini kwa mara nyingine ilishindwa kufanya hivyo. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Mjibu Shauri alishindwa kutimiza wajibu wake wa kujitetea, hatimaye, bila kuombwa na Mleta Shauri, Mahakama, kwa hiari yake, iliamua kutoa uamuzi wa moja kwa moja.

Kisha Mahakama iliangalie endapo ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo. Katika suala hili, Mahakama ilibaini kuwa ilikuwa na mamlaka binafsi kwani Mjibu Shauri ni mhusika wa Itifaki na alikuwa ameweka Azimio chini ya Kifungu cha 34(6) cha Itifaki kwenye Tume ya Umoja wa Afrika tarehe 29 Machi 2010. Ingawa Mjibu Maombi baadaye aliondoa Azimio lake mnamo tarehe 21 Novemba 2019, Mahakama ilisisitiza kwamba uondoaji huo hautekelezwi kwa kurudi nyuma na unaanza kutumika ndani ya mwaka mmoja baada ya taarifa ya uondoaji kuwasilishwa. Kwa kuwa tarehe ya kuanza kutekelezwa uondoaji huo ilikuwa tarehe 22 Novemba 2020 na Shauri hili liliwasilishwa tarehe 25 Julai 2016, Mahakama iliona kwamba mamlaka yake binafsi yalithibitishwa.

Mahakama pia iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya kisheria kwa kuwa Mleta Shauri alikuwa amedai ukiukaji wa Kifungu cha 2, 3, 7(1), 9(1), 14, na 16 cha Mkataba, ambao Mjibu Shauri ni mhusika. Mahakama pia iliona kwamba ilikuwa na mamlaka ya muda,

kwa kuwa ukiukaji unaodaiwa kufanywa uliotokea kati ya mwaka 2002 na 2017, ulikuwa umeanza kabla ya mwaka 2006, wakati ambapo Mjibu Shauri aliridhia Itifaki, lakini uliendelea baada ya hapo. Mwisho, Mahakama iliona kuwa ilikuwa na mamlaka ya kieneo, ikizingatiwa kuwa ukweli wa kesi hiyo ulitokea ndani ya eneo la Mjibu Shauri, ambaye ni mhusika wa Mkataba na Itifaki. Kulingana na mambo yaliyotajwa hapo juu, Mahakama ilihitimisha kwamba ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Kisha Mahakama iliangalia endapo Maombi hayo yalikuwa yanakubalika. Katika suala hili, iliona kwamba, Mleta Shauri alikuwa ametambuliwa dhahiri kwa jina kwa kutimiza Kanuni ya 50(2)(a) ya Kanuni za Mahakama. Iliona pia kwamba madai ya Mleta Shauri yalilenga kulinda haki zake kulingana na Kifungu cha 3(h) cha malengo ya Sheria ya Kikatiba ya Umoja wa Afrika, na hivyo Shauri hilo lilizingatia Kanuni ya 50(2)(b) ya Kanuni za Mahakama. Aidha, Mahakama ilibaini kuwa lugha iliyotumiwa katika Shauri hilo haikuwa ya kudharau au kumtukana Mjibu Shauri au taasisi zake, au Umoja wa Afrika katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(c) ya Kanuni za Mahakama na pia kwamba Maombi hayakuzingatia tu habari zilizosambazwa kupitia vyombo vya habari katika kutimiza Kanuni ya 50(2)(d) ya Kanuni za Mahakama.

Kuhusiana na kukamilisha taratibu za ndani, Mahakama iliona kwamba Mleta Shauri alikuwa hajatoa ushahidi wa kutosha kuthibitisha madai kwamba alikuwa na kesi inayoendelea ambayo ilichukua muda mrefu isivyo lazima. Pia ilibaini kwamba Mleta Shauri hakueleza ni kwa nini hakukata rufaa dhidi ya amri ya kufukuzwa nchini ingawa alikuwa amepewa dhamana na Mahakama ya Wilaya.

Kuhusiana na hoja yake kwamba hadhi yake ya "wahamiaji waliopigwa marufuku" ilimfanya ashindwe kukamilisha taratibu za ndani, Mahakama ilibaini kwamba Mleta Shauri hakuwa ameonyesha kwamba alikuwa amejaribu kufungua kesi katika nchi ya Mjibu Shauri kupitia mwakilishi wa kisheria na kwamba alikataliwa. Kwa hivyo, Mahakama iliona kwamba Mleta Shauri alikuwa ameshindwa kukamilisha taratibu zote za ndani, na kwa sababu hiyo, Maombi haya hayakuzingatia Kifungu cha 56(5)

cha Mkataba, kama ilivyoonyeshwa katika Kanuni ya 50(2)(e) ya Kanuni za Mahakama.

Mahakama iliona kwamba haikuwa muhimu kuangalia matakwa ya Kifungu cha 56(6) na 56(7) cha Mkataba, kwa kuwa masharti ya ukubalifu ni jumuishi. Matokeo yake, Mahakama ilitangaza kwamba Maombi hayo hayakuwa yanakubalika.

Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake.

**Maelezo zaidi**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, yanaweza kupatikana kwenye tovuti kupitia: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0142018

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*